

HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA



KUMB. NA. UDC/ADM/A. 10/190/VOL. V/5

20/11/2021

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga anapenda kuwatangazia waombaji walioorodheshwa hapo chini, walioomba nafasi ya kazi ya Mtendaji wa Kijiji kwa kibali cha Ajira Mbadala Kumb Na. FA.170/361/01 "A"/162 cha tarehe 10/09/2021, wamechaguliwa kuhudhuria usaili utakaofanyika katika shule ya msingi Mahenge kuanzia siku ya Jumanne tarehe **30/11/2021 hadi siku ya Jumatano tarehe 01/12/2021 saa 2:00 Asubuhi**. Aidha usaili wa mchujo (Written Interview) utafanyika siku ya Jumanne tarehe 30/11/2021, na wasailiwa watakaofaulu ndio watakaochaguliwa kuendelea na usaili wa mahojiano (Oral Interview) siku ya Jumatano tarehe 01/12/2021 katika ukumbi wa Halmashauri (Pauline Hall) kuanzia saa 2:00 Asubuhi. Usaili utafanyika kwa njia ya maandishi na Mahojiano kwa wote na usaili wa vitendo kwa madereva.

Kwa waombaji ambao majina yao hayakuonekana katika orodha hapo chini watambue kuwa maombi yao hayajakidhi sifa kwa mujibu wa nafasi zilizotangazwa. Mkurugenzi Mtendaji Wilaya anawashukuru kwa kuleta maombi yao na kuwataka wasisite kutuma maombi tena pindi Halmashauri itakapotangaza nafasi za kazi.

Masharti ya Usaili:

- Wasailiwa wote wanatakiwa wawe na namba za utambulisho wa Utaifa (NIDA)
- Wasailiwa wafike na Vyeti Halisi (Original) vya Taaluma, cheti cha Kuzaliwa, Vyeti vya Shule na kwa wasailiwa wa nafasi ya udereva waje na leseni halali ambayo haijaisha muda wake.
- Wasailiwa wote wawe na kitambulisho au barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Mtaa au Kijiji anachotoka. Vitambulisho vikakavyokubaliwa ni pamoja na Kitambulisho cha Uraia, kitambulisho cha Mpiga kura, Leseni ya udereva au Pasi ya Kusafiria.
- Msailiwa anayekuja kufanya usaili atajigharamia mwenyewe.

Msailiwa anatakiwa kuzingatia tarehe, muda na eneo la usaili
Usaili utafanyika kwa njia ya maandishi na mahojiano

